

HALMASHAURI YA MJI WA KONDOA

(Barua zote zitumwe kwa Mkurugenzi Halmashauri ya Mji wa Kondoa)

Simu: +255 712264912

Nukushi: +255 262360313

Barua pepe:

td@kondoatc.go.tz



Mkurugenzi wa Mji
S.L.P 711,
KONDOA.

TAARIFA YA IDARA YA MIPANGO

1.0 UTANGULIZI

Idara ya mipango ni moja ya Idara ambayo ni kiungo cha Halmashauri ambacho kazi yake kubwa ni kupanga, kuchambua sera mbalimbali za serikali, kukusanya na kutunza takwimu za Halmashauri ikiwa ni pamoja na kuandaa bajeti ya Halmashauri.

Kupanga ni Kuchagua au ni mchakato endelevu unaohusisha kuweka vipaumbele na kufanya uamuzi katika kuchagua mbinu mbadala na kutumia rasilimali zilizopo kwaajili ya kutimiza malengo fulani wakati ujao. Kupanga kunahusisha mambo yafuatayo;

- ✓ Kuchukua maamuzi, kuweka vipaumbele na kuchagua
- ✓ Kuandaa rasilimali
- ✓ Kuweka lengo na madhumuni
- ✓ Kulenga wakati ujao

Tunapopanga tunajibu maswali yafuatayo

- ✓ Tunapanga kwaajili ya nani? (Who)
- ✓ Tunapanga wapi? (Where)
- ✓ Tunapanga nini? (what)

- ✓ Tunapanga lini? (when)
- ✓ Tunapanga namna gani? (how)

Mpango wa Halmashauri ni Mpango wa Kiuchumi na Kijamii unaotumia njia shirikishi kuanzia chini kwenda juu kwenye Vijiji na mitaa hadi Halmashauri.

Watumishi wa Kitengo cha Mipango, Takwimu na Ufuatiliaji

- ✓ Afisa Mipango (Mchumi)
- ✓ Mtakwimu
- ✓ Katibu Muhtasi
- ✓ Dereva

1.1 Wadau wanaohusika katika Mipango ya Halmashauri

i. Halmashauri ya Mji ni Mamlaka ya Mipango iliyowekwa kwa mujibu Kifungu cha 36 (1) cha sheria ya serikali za mitaa mwaka 1997 ambayo ilipitiwa mwaka 2001. Halmashauri inatengeneza sera ambamo Mipango yake hujikita

ii. **Kamati ya Mipango ya Halmashauri;** Hii ni kamati ya kitaalamu ambayo inaundwa na Wakuu wa Idara ikiongozwa na Mkurugenzi. Kamati za Idara huandaa Mipango ya kisekta na wakuu wao Idara au Vitengo vyao ambapo Kitengo cha Mipango kina mamlaka ya kuratibu uandaaji wa Mipango hiyo.

iii. **Kamati za kisekta ndizo zinazohuisha sera za halmashauri**

iv. Kamati za Mipango ngazi ya kata na Vijiji au Mitaa zikiongozwa na Diwani na Mtendaji wa Kata akiwa ni katibu wa kamati hiyo ya Maendeleo (WDC)

1.2 Mchakato wa Uandaaji Mipango (Planning Process)

Mchakato wa kupanga huanzia ngazi ya kijiji au mtaa ambapo vipaumbele huandaliwa kupitia mbinu shirikishi ya Mfumo Ulioboreshwa wa Fursa na Vikwazo kwa Maendeleo (Improved O&OD) ambapo vipaumbele huibuliwa kupitia kushirikisha wananchi ngazi ya Vijiji na mitaa na hatimae kuwasilishwa katika ngazi ya Kata ambako hujadiliwa na Kamati ya Maendeleo ya Kata (WDC). Baada ya kujadiliwa vipaumbele hivyo huwasilishwa ngazi ya Halmashauri kwaajili ya kuchambuliwa katika Kitengo cha Mipango na kuwasilishwa katika Kamati ya Mipango ya Halmashauri ya Mji. Baada ya uchambuzi kupitia kamati ya Mipango ya Halmashauri Vipaumbele hivyo hujumuishwa katika Mpango wa Halmashauri ya Mji.

1.3 Ufuatiliaji na Tathimini (M&E)

Usimamizi na ufuatiliaji umekua haufanyiki kwa wakati kutokana na kuchelewa kwa kutolewa kwa fedha kutoka serikali kuu na hatimaye kuchelewa kwa utekelezaji. Hii imefanya kuwe na mapitio ya mara kwa mara na kuwa magumu na kutokuwa na uhalisia. Hii inaweza kwisha iwapo hela zitatolewa kwa wakati.

2.0 MAWASILIANO YA WATUMISHI WA IDARA AU KITENGO

Kitengo hiki kina watumishi watatu kwasasa ambao ni

Na	Jina	Cheo	Na.ya Simu
1.	Nyange Athumani Siraji	Afisa Mipango	0785 888 774
2.	Mashaka Andrew Mkongwa	Mchumi	0788 777 611
3.	Abdul	Mtakwimu	0715 738 321

3.0. KAZI ZA IDARA

Idara ya mipango inafanya kazi mbalimbali ili kutimiza majukumu yake ya kilasiku nazo ni kama ifuatavyo:

- i. Kusimamia utekelezaji wa mpango na bajeti kwa kila Idara
- ii. Kukusanya takwimu na taarifa mbalimbali za kiuchumi kwa ajili ya uchambuzi na uaandaji wa sera na Mipango ya kiuchumi na kijamii
- iii. Kufanya utafiti juu ya masuala mbalimbali yatokanayo na utekelezaji wa sera za kiuchumi
- iv. Kufanya utafiti na uchambuzi wa sera na vigezo vya uchumi jumla
- v. Kufanya utafiti na kubainisha fursa zilizopo katika sekta husika
- vi. Kukusanya taarifa na takwimu zinazohitajika katika kubainisha vipaumbele vya ustawi na maendeleo ya jamii.
- vii. Kutayarisha na kusambaza takwimu na taarifa za kiuchumi kwa Washikadau
- viii. Kuchambua na kutafsiri (interpret) takwimu na taarifa mbalimbali
- ix. Kufanya utafiti na kubainisha fursa zilizopo katika sekta husika
- x. Kuainisha vipaumbele vya maendeleo
- xi. Kuandaa ratiba ya kazi zinazohusika (Action Plan)
- xii. Kufanya tathmini ya sera za sekta

- xiii. Kubuni na kuweka mikakati ya kuongeza ufanisi katika uzalishaji na utoaji huduma
- xiv. Kutathmini muundo wa serikali wa utoaji huduma mbalimbali za jamii na utawala
- xv. Kutathimini ujuzi na uwezo binafsi wa watumishi wa Idara mbalimbali katika kutoa huduma kwa ufanisi na kutoa ushauri
- xvi. Kubuni na kuweka mikakati ya kuongeza ufanisi katika kutoa huduma
- xvii. Kutathimini na kuweka vipaumbele katika maeneo ya kuwekeza katika sekta za uzalishaji, miundombinu na maendeleo ya jamii na utawala
- xviii. Kuhifadhi takwimu na taarifa kuhusu mwenendo wa utendaji na utoaji wa huduma
- xix. Kuwa na mashauriano ya kitaalam katika sekta husika
- xx. Kusaidia katika kuandaa taarifa ya utekelezaji wa kazi anazofanya kwa mwaka
- xxi. Kutoa ushauri wa kitaalam juu ya upangaji wa masuala ya rasilimali watu
- xxii. Kutambua mahitaji ya utalam katika sekta za jamii
- xxiii. Kuongoza katika kuandaa/ kutayarisha makala ya maendeleo ya Rasilimali watu
- xxiv. Kutoa ushauri kuhusu mikakati ya ukuaji ajira

- xxv. Kutathimini mahitaji na matokeo ya taasisi za mafunzo kulingana na soko la ajira
- xxvi. Kuchumbua takwimu na taarifa mbalimbali za kiuchumi na kuandaa sera za uchumi jumla na Mipango ya maendeleo ya Mji
- xxvii. Kutayarisha taarifa za mapitio ya mwenendo wa kiuchumi na kijamii za robo na nusu mwaka
- xxviii. Kuchambua mwenendo wa bajeti ya Mji na Idara ya Mipango
- xxix. Kuandaa mfumo/mtindo wa uchambuzi wa makisio ya vigezo vya uchumi jumla

4.0. HUDUMA ZITOLEWAZO KATIKA IDARA

Idara ya Mipango inatoa huduma mbalimbali kwa wananchi wa Halmashauri ya Mji Kondoa ikiwemo;

- i. Taarifa mbalimbali za maendeleo kupitia wawakilishi wao kwenye vikao vya Kamati na mabaraza na mbao za matangazo
- ii. Ushauri na kuwashirikisha wananchi katika kuibua fursa mbalimbali za kimaendeleo
- iii. Kutoa elimu kwa wananchi juu uibuaji wa miradi yenye tija kimaendeleo katika jamii
- iv. Kutoa ushauri katika sekta binafsi katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo ili waweze kufuata sera za kimaendeleo za taifa na wilaya

- v. Kupata miongozo, sera, mpango mkakati na malengo ya Halmashauri katika kuleta maendeleo kwa wananchi

5.0. MATARAJIO YA IDARA AU KITENGO

- i. Kuwajengea uwezo wananchi katika kuibua miradi yenye tija katika kuleta maendeleo
- ii. Kuendelea kuboresha huduma za jamii kwa kusimamia kikamilifu miradi ya maendeleo
- iii. Kuendelea kutoa wigo mpana kwa wananchi katika kupanga kwa kuwashirikishi katika kuibua miradi na kutekeleza

KARIBUNI SANA KATIKA IDARA YA MIPANGO